KANUNI NA MASHARTI YA FOSA

TANESCO SACCOS

1.MAWANDA NA MATUMIZI

Kanuni na masharti haya yanaunda mkataba kati ya mteja na TANESCO SACCOS . Mteja ataomba kwa TANESCO SACCOS kwa kutumia fomu hii iliyotolewa kwa kuendesha akaunti na kutumia huduma zinazohusiana. Kwa kuomnba kufungua akaunti, mteja anatakiwa kusoma, kuelewa na kukubali kanuni na masharti haya. Kwa nyongeza, kanuni na masharti mahususi yoyote yanayohusika na ada zilizowekwa katika mwongozo na ushuru vitatumika. Katika hali ya mwingiliano wowote kati ya kanui na masharti na kanuni mahususi na zinazohusian na bidhaa maalumu yeyote au akaunti, kanuni na masharti mahususi yanayohusika vitatumika

2.FASILI

Katika kanuni na masharti haya, maneno na kauli zitakua na maana zilizoelezwa hapa chini isipokua kama itaelezwa vinginevyo.”Akaunti” ina maana akaunti iliyofunguliwa na kuendelezwa kwa mujibu wa maelezo ya upande wa pili na akaunti nyingine yoyote iliyofunguliwa na mteja TANESCO SACCOS.

ATM ina maana mashine inayojiendesha yenyewe ‘TANESCO SACCOS ’ ina maana Chama cha ushirika wa akiba na mikopo cha TANESCO ikiwa na ofisi yake ya usajili Dar Es Salaam.

’Kadi’ ina maana kadi ya elektroniki ya kutolea fedha inayotolewa na TANESCO SACCOS na maombi na kwa jina la mtu aliyeandikwa kwenye kadi kwa matumizi yanayohusiana na huduma za kadi ya kutolea fedha zinazotolewa

‘Mwenye kadi’ ina maana mtu ambaye kadi yake inapaswa kutolewa fedha kulingana na kumbukumbu za kadi na kwa yule aliyepewa kadi. Majina yao pia yanaandikwa kwenye kadi na wanakubali kufata kanuni na masharti kama yatakavyobadilika mara kwa mara

‘Mteja’ ina maana mtu yeyote mwenye akaunti TANESCO SACCOS.

‘Huduma’ ina maana huduma zinazotolewa na TANESCO SACCOS zinazohusiana na hasa zaidi zilizoelezwa katika masharti haya.

‘Pin’ ina maana namba ya utambulisho binafsi inayochaguliwa na mwenye kadi kwa ajili ya matumizi ya kadi yake.

3. UFAFANUZI

a)Marejeo yote yaliyo katika umoja yanajumuisha wingi na vivyo hivyo kinyume chake na neno “kujumuisha” linapaswa kutafsiriwa kama “bila ya kikomo”.

b)Neno linalomaanisha jinsia yeyote linajumuisha jinsia nyingine.

c)Marejesho kwa sheria yeyote ya kampuni, sheria au sheria nyingine yanajumuisha kanuni zote za hati nyingine na uunganishaji wote, marekebisho, utungaji upya au ubadilishajiwa sheria kwa wakati inapokua katika utekelezaji.

d) Vichwa vya habari vyote, uchapaji kwa herufi nzito na italiki (kama upo) vimeingizwa kwa ajili ya kurahisisha marejeo.

4. MAREKEBISHO YA KANUNI NA MASHARTI

TANESCO SACCOS itakua na uamuzi wa mwisho wa kurekebisha au kuongeza kanuni na masharti yeyote mahususi (ikiwa ni pamoja na viwango vya riba na gharama zozote za TANESCO SACCOS) wakati wowote. Mteja atafahamishwa kuhusiana na mabadiliko yeyote kwa namna itakayoamuliwa na TANESCO SACCOS

5. KUFUNGUA AKAUNTI; kumbukumbu za kutoa

5.1 Ili kufungua akaunti TANESCO SACCOS , waombaji lazima (i) wajaze fomu inayohusika na maombi inayotolewa na TANESCO SACCOS ili kuwe na majibu sahihi na ya kina kwa maswali yote yanayoulizwa na TANESCO SACCOS (ii) waambatanishe nyaraka zote zilizotajwa katika fomu hiyo ya maombi; na (iii) watoe taarifa nyingine zote kama hizo au nyaraka zitakazoombwa na TANESCO SACCOS

5.2 Mwombaji lazima athibishwe na mtu wa tatu anayeaminika, ambae utambulisho wake utakubaliwa na TANESCO SACCOS kabla, na TANESCO SACCOS ina haki ya kutafuta na kuchukua kumbukumbu kwa waombaji hao

5.3 TANESCO SACCOS inapopokea mambi ya kufungua akaunti na baada ya hapo wakati wowote inaweza kuuliza kuhusu kumbukumbu za mkopo kwa mteja na mashirika ya mkopo au watu wengine kama TANESCO SACCOS itaona ni muhimu au inafaa

5.4 Ni pale tu TANESCO SACCOS itakapothibitisha kwa mteja kuhusu mafanikio ya utambulisho wake na kurekodi data zake TANESCO SACCOS itafungua akaunti kwa ajili ya mteja.

5.5 Pale mteja atakapotoa maombi ya maandishi kwa TANESCO SACCOS , TANESCO SACCOS inaweza (lakini haitalazimishwa) kutoa taarifa kwa mashirika ya mikopo na taasisi nyingine kwa kuzingatia uendeshaji wa akaunti yeyote ya mteja kwa TANESCO SACCOS haitaingia deni kwa kufanya ivyo.

6. WATIA SAINI WALIOIDHINISHWA

Mteja atatoa sampuli ya saini za wateja na maelezo ya watia saini walioidhinishwa (na atahakikisha kwamba mtia saini yoyote aliyeidhinishwa anatoa sampuli ya saini), kama na wakati atakapohitajiwa kufanya hivyo na TANESCO SACCOS .

7. UTUNZAJI SALAMA

Mteja pekee atawajibika na utunzaji salama wa taarifa za akaunti, cheti cha taarifa za Salio, kadi, PIN na vitu vingine kama hivyo vinavyohusiana na kufungamana na akaunti.

8. UENDESHAJI WA AKAUNTI

a. Miamala kwa kawaida hufanywa katika saa za kazi TANESCO SACCOS au katika matawi yoyote ya Benki ya Posta Tanzania . TANESCO SACCOS haitahusika katika uchelewaji wowote katika akaunti yoyote kwa kushindwa kuunganishwa

b. TANESCO SACCOS kwa uamuzi wake pekee inaweza kuzuia idadi ya utoaji fedha katika akaunti.

9. KUTOA MAELEKEZO

9.1 TANESCO SACCOS itashughulikia maelekezo yanayotolewa katika hati yenye saini halisi ya mteja (au mtia saini wake aliyeidhinishwa)

9.2 TANESCO SACCOS kwa uamuzi wake, katika mazingira Fulani inaweza kuruhusu maelekezo yatolewe kwa njia ya simu, barua pepe, nakala halisi au njia nyingine ilimradi taratibu za TANESCO SACCOS za usalama zimefuatwa.

9.3 TANESCO SACCOS inaweza kukataa kushughulikia maelekezo yoyote kama maelekezo hayo yatakuwa hayaeleweki, au kama TANESCO SACCOS inaamini kwamba (i) kufanya ivyo kutaingilia sheria au kanuni yoyote inayotumika au (ii)TANESCO SACCOS kwa nia njema inaamini kwamba maelekezo yanaweza kuhusisha udanganyifu au mwenendo wowote mbaya wa uhalifu.

10 WAMILIKI WA AKAUNTI YA PAMOJA

10.1 Pale ambapo akaunti itafunguliwa na kuendeshwa kwa jina la zaidi ya mtu mmoja, haki na wajibu wa mmiliki wa akaunti ya pamoja na mambo mengine kutegemeana na uendeshajiwa akaunti yatakua kama yalivyokubaliwa kwa maandishi na kila mmoja wao na TANESCO SACCOS kwa mara kwa mara.

10.2 Kama hakutokuwapo makubaliano kinyume na kifungu 10.1, wamiliki wa akaunti watakua na dhima pamoja au baadhi na kila mmiliki wa akaunti ya pamoja atachuchukuliwa kuwa na mamlaka kamili ya kuendesha akaunti, kutoa na kuhamisha fedha kutoka kwenye akaunti ya pamoja bila ridhaa ya wamiliki wengine wa akaunti

10.3 Marejeo ya “mteja” katika marejeo na masharti haya yatajumuisha kila mmiliki wa akaunti ya pamoja

11. AKAUNTI ISIYOTUMIKA

11.1 TANESCO SACCOS inaweza kuainisha akaunti kama isiyotumika endapo hakuna mteja anayetumia kwa miezi 12. Mteja kutumia akaunti itamaanisha kuingiza kokoe fedha na kutoa kunakofanywa na mteja katika akaunti yake kupitia njia zifuatazo

i. Kuweka/Kutoa fedha

ii. Kutoa fedha kupitia ATM

11.2 TANESCO SACCOS kwa uamuzi wake pekee inaweza kuzuia huduma na/au shughuli katika akaunti ya mteja ambayo imeainishwa kama isiyotumika

12 MABADILIKO YA MAELEZO YA MTEJA

Mteja anapaswa kuiarifu TANESCO SACCOS mara moja kwa maandishi (au kwa uamuzi wa TANESCO SACCOS au nyingine yoyote) kuhusu mabadiliko yoyote ya jina au makazi, anwani ya mawasiliano (katika kila namna akitoa ushahidi kama TANESCO SACCOS inavyohitaji) Au ufutaji wowote au mabadiliko katika uidhinishaji wowote unaofanywa na mteja huyo.

13. HUDUMA YA UCHUKUAJI

Hundi, hawala, bili, gawio/riba na hati nyingine zinatolewa kwa maslahi ya mteja zinazokubaliwa kuchukuliwa kwa niaba ya mteja. Uchukuaji wa hati ya nje ya TANESCO SACCOS unaingiza gharama za uchukuaji.

a) TANESCO SACCOS haikubali jukumu lolote la upotevu,ucheleweshaji, uondoaji maneno na uzuiaji wa hati katika posta au kwa mtu anaepeleka barua. TANESCO SACCOS wala kushirikina jukumu lolote kwa uchelewaji wa kupata hati izo au kwa uhalisia , uhalali, au usahihi wa saini au uidhinishaji uliomo. Utoaji fedha kwa kutumia hati izo unaruhusiwa tu kwa kutambuliwa kwa utaratibu wa TANESCO SACCOS .

b) TANESCO SACCOS ina mamlaka ya kutoa fedha kwenye akaunti ili kulipia kiasi chochote kilichotolewa kimakosa kwenye akaunti ya mteja.

c) Endapo hundi itarejeshwa, kiasi ambacho kimeishaingizwa kwenye akaunti ya mteja na/au kuhusiana na utoaji wa fedha usioruhusiwa, TANESCO SACCOS itabadilisha uingizaji wa kiasi hicho na kukata kiasi kinacholingana na kiasi kilichokatika hundi iliyorejeshwa. Kwa matukio kama hayo, kama akaunti haitakuwa na fedha za kutosha, kiasi kilichobakia kitachukuliwa kuwa deni la muda linalodaiwa kwa mteja na mteja atalazimika kulipa kiasi hicho haraka atakapotakiwa kufanya hivyo na TANESCO SACCOS

14. KIFO AU KUTOJIWEZA

Mteja anakubali kuiarifu TANESCO SACCOS kwa haraka kama yeyote kati ya mmiliki wa pamoja wa akaunti au mtia saini aliyeidhinishwa katikaakaunti amefariki au mahakama imetamka kuwa hajiwezi . TANESCO SACCOS inaweza kusitisha akaunti na kusimamisha shughuli zote pale ambapo yeyote kati ya wamiliki wa akaunti ya pamoja au watia saini walioidhinishwa watafariki au kutajwa kuwa hawawezi. TANESCO SACCOS inaweza kuendeleza usitishaji wa akaunti hadi itakapopata utambulisho na/au utambulisho wa warithi/wanufaika kwa kuridhika kwake

15. KUTOHAMISHIKA

Akaunti na huduma zinazotolewa kwa mteja hazihamishiki katika mazingira yoyote na zitatumika na mteja tu. Hata hivyo, TANESCO SACCOS itakuwa na haki ya kuhamisha, kutoa au kuuza haki zote, marupurupu au wajibu kwa yeyote na masharti haya yataendelea kutumika kwa manufaa ya warithi na kazi za TANESCO SACCOS .

16. TAARIFA

Taarifa zinazohusiana na akaunti, huduma na shughuli nyingine zinazohusiana na akaunti zinaweza kutolewa na TANESCO SACCOS ama kwenye tawi au kwa kutumia barua kwenye anwani ya mteja. Taarifa zote kuhusiana na huduma au akaunti zinatolewa na mteja kwa TANESCO SACCOS zitakuwa kwa maandishi na kupelekwa kwenye tawi la TANESCO SACCOS ambako mteja alifungua akaunti na taarifa zote zitachukuliwa kuwa zimepokewa na TANESCO SACCOS baada tu ya kukubali kupokelewa kwa maandishi na TANESCO SACCOS .

17. MIAMALA KUPITIA ELECTRONIKI

TANESCO SACCOS inaweza kutoa huduma kupitia ATM, taarifa kupitia ujumbe wa simu, huduma za TANESCO SACCOS jongezi na huduma za TANESCO SACCOS kwa njia ya internet kwa mteja. Mteja atakubali kufuata na kukubaliana na kanuni na masharti yote hayo kama TANESCO SACCOS itakavyoeleza mara kwa mara, na hapa anakubali na kuthibitisha kuwa miamala yote itakayofanywa kwa njia ya electroniki, compyuta, mtandao wa mashine inayojiendesha au kupitia njia nyingine za mawasiliano ya simu zilizoanzishwa na au kwa niaba ya TANESCO SACCOS kwa ajili ya kuhusiana na akaunti, au bidhaa na huduma nyingine za TANESCO SACCOS , zitaunda KISHERIA MASHARTI na uhalali wa miamamala inayofanywa kwa kufuata na kwa kutekeleza kanuni na masharti ya TANESCO SACCOS kwa huduma izo, kama itakavyoelezwa mara kwa mara.

18. UKOPAJI WATEJA

18.1 Mteja ataweza kukopa kutoka TANESCO SACCOS pale tu masharti yaliyokubaliwa kwa maandishi kati ya mteja na TANESCO SACCOS yatazingatiwa.

18.2 Huduma yoyote kama hiyo lazima iidhinishwe kwanza na TANESCO SACCOS katika kila tukio. Mwombaji anakubali kwamba masharti ya huduma yoyote au ufadhili vinaweza kutolewa au kukataliwa kwa uamuzi pekee wa TANESCO SACCOS .

18.3 TANESCO SACCOS itatoa riba katika deni lolote katika akiba au huduma nyingine, mchanganyiko au moja kama itakavyoamuliwa katika uamuzi pekee wa TANESCO SACCOS (au kama itakavyokubaliwa kipekee kwa maandishi na mteja) mteja anakubali bila kubadilisha na bila masharti kulipa riba yoyote au yote kwa TANESCO SACCOS kama na wakati na wa njia yoyote TANESCO SACCOS inavyoamua au kuagiza

18.4 Wateja watawajibika kwa kiasi chochote wanachodaiwa na TANESCO SACCOS .

19. MALIPO YA RIBA

Riba inalipwa katika kiwango kinachozidi salio la chini la mkopo kinachoendelezwa katika kipindi Fulani kitakachoamuliwa na TANESCO SACCOS .

20. GHARAMA, ADA NA MATUMIZI, MAKATO KUTOKA KWENYE AKAUNTI

20.1 TANESCO SACCOS itakua na haki ya kutoza ada ya matumizi kama ilivyoelezwa katika mwongozo wa tozo, kila ada itatofautiana mara kwa mara.

20.2 TANESCO SACCOS itakua na haki (bila kuwasiliana na mteja) kutoa fedha katika akaunti yoyote ya mteja kuhusiana na ada yoyote, matumizi (ikijumuisha, bila ya kikomo, gharama za sheria, kodi na ushuru wa stempu) riba, kamisheni zinazolipwa au zinazotumika kwa niaba yake au gharama au gharama zinazotozwa kama matokeo ya shughuli yoyote kati ya TANESCO SACCOS na mteja.

21. UMILIKI UANZISHWAJI WA TANESCO SACCOS

22.1 Kwa kuongeza umiliki wowote wa jumla au haki nyingine au marekebisho ambayo TANESCO SACCOS inaweza kustahili iwe kwa uendeshaji wa sheria au vinginevyo TANESCO SACCOS , wakati wowote , na bila ya taarifa inaweza kuunganisha au kuweka pamoja akaunti yoyote au akaunti zote za mteja katika fedha yoyote au kuweka au kuhamisha kiasi chochote kilichobakia katika mkopo wa akaunti yoyote katika kulipia madeni yoyote ya mteja kwa TANESCO SACCOS yanayohusiana na akaunti nyingine yoyote au yanayohusiana na jambo jingine lolote, bila ya kujali kama madeni hayo ni mengi au ya pamoja.

21.2 TANESCO SACCOS itakua na umiliki katika madai yote ambayo mteja anastahili au ambayo mteja atastahili yatakayotokana na uhusiano kati ya TANESCO SACCOS na mteja

21.3 Umiliki utakua kama dhamana kwa madai yote yaliyopo, ya baadae na masharti dhidi ya mteja, ambapo TANESCO SACCOS inastahili kutokana na uhusiano wa shughuli za TANESCO SACCOS .

22. KUVUNJA UHUSIANO

22.1 Wakati wowote na bila ya kutoa sababu yoyote kwa taarifa ya maandishi, mteja anaweza kuvunja ama uhusiano wote na TANESCO SACCOS au huduma maalumu zinazohusiana na bidhaa maalum (kwa suala la umiliki wa pamoja,wamiliki wote wa akaunti lazima watie saini), uvunjaji huo usiwe na athari kwa haki zozote zinazotokana na kipindi cha kuvunja.

22.2 Wakati wowote na bila kutoa sababu yoyote baada ya kutoa taarifa ya maandishi ya siku 30 baada ya kuvunja uhusiano wote na TANESCO SACCOS au mteja au huduma nyingine maalumu, uvunjaji huo usiwe na athari kwa haki zozote zinazokuwapo katika kipindi cha uvunjaji.

Hata hivyo, TANESCO SACCOS itastahili kuvunja uhusiano wote na mteja mara moja kama ina amini vya kutosha kwamba (i) mteja amekua akijihusisha katika tabia za udanganyifu au tabia nyingine za uhalifu (ii) kuna masharti ya kanuni na masharti au kanuni na masharti yoyote mahsusi ambayo yamevunjwa (iii) uhusiano kati ya TANESCO SACCOS na mteja yamevunjika au (iv) mteja (ikiwa) mmiliki yoyote wa pamoja anayeunda sehemu ya mteja ameamuliwa kufilisiwa, amefilisika au masuala yao yamekuwa ya kiutawala, usimamizi au mchakato mwingine unaofanana na huo

22.3 Kwenye ufunguaji wa akaunti yoyote, mteja atarejesha vitu kama ambavyo atatakiwa na TANESCO SACCOS (ikiwa ni pamoja na, bila kikomo kadi zote na hundi ambazo hazijatumiwa). Mteja mara moja atalipachochote kilichobakia kwa ajili ya TANESCO SACCOS.

23. DHIMA.

23.1 Katika kanuni na masharti haya, uondoaji au uuzaji wa dhima au marekebisho yatafaa tu kwa kiasi kwamba dhima au marekebisho:

23.1.1 Hayatokani na kifo au madhara ya mtu binafsi

23.1.2 Yanaweza kisheria kuondolewa au kuwa na ukomo, na

23.1.3 Hayatokani na udanganyifu au ukosaji wa uaminifu wa mtu huyo anayehusika na uondolewaji au uzuiaji
23.2 Si TANESCO SACCOS , maofisa wake, mawakala au waajiri watawajibika kwa utoaji usioidhinishwa kutoka au ufikiaji wa akaunti yoyote isipokua ambapo taarifa ya awali ya upotevu wa taarifa yoyote ,fomu ya kutolea au rekodi ya akaunti nyingine itatolewa kwa TANESCO SACCOS na kuthibitishwa kwa maandishi.
23.3 Ushahidi wowote wa maandishi utakaotolewa na TANESCO SACCOS kuhusiana na akaunti ya mteja utachukuliwa kuwa ndio wa mwisho na ushahidi wa kuthibitisha hali ya akaunti ya mteja
23.4 TANESCO SACCOS haitawajibika kwa mteja kwa kushindwa kokote kutimiza masharti yoyote yanayosababishwa na hali zozote nje ya udhibiti wake mzuri au kwa kushindwa kutenda kulingana na ibara ya 9.3
24.5 Dhima ya TANESCO SACCOS kwa mteja kwa hasara au madhara yanayotokana na kushindwa ,kuchelewa au kosa katika kufuata maelekezo katika tukio lolote utawekewa kikomo kwenye kiasi cha chini cha hasara au madhara hayo na kiasi cha faida yoyote ambayo haikupokelewa au kulipwa na mteja kutokana na kushindwa huko,ucheleweshaji au kosa.
TANESCO SACCOS haitawajibika kwa mteja kwa hasara ya biashara upotevu wa imani ,upotevu wa fursa,upotevu wa faida au aina yoyote nyingine ya hasara maalumu ,inayoandamana au ya moja kwa moja
23.6 TANESCO SACCOS haitawajibika kwa hasara zozote ambazo mteja ameingia kwa njia isiyo ya moja kwa moja au ambazo TANESCO SACCOS isingeweza kuzitabiri.
23.7 TANESCO SACCOS haitawajibika kwa mteja kuhusiana na uchukuaji wa hatua yoyote inayohitajika kisheria ,ikiwa ni pamoja na,bila ukomo ,kufuata agizo lolote la kuzuia Akaunti ya mteja au agizo la jaji la uzuiaji wa akaunti ya mteja kutolipa pesa kwa mwia/mdai 1 mpaka kwa amri ya mahakama

24.HATI YA KUSAMEHE MADENI
Hakuna kushindwa au kuchelewa kwa TANESCO SACCOS katika utekelezaji wa haki yeyote.Uwezo /Madaraka au Marupurupu ambayo yametajwa hapa yataendeshwa kama hati ya kusamehe madai katika jambo pekeeau kama sehemu ya haki nyingine,madaraka au marupurupu.
Haki na marekebisho ya TANESCO SACCOS kama yalivyoelezwa hapa yatakua ya kulimbikiza na siyo pekee kwa haki zozote au marekebisho yaliyotolewa kisheria.

25.FIDIA
a) Mteja hapa anakubali kwamba,yeye mteja kwa gharama zake mwenyewe atafidia kulinda na kusimamia TANESCO SACCOS isiingie hasara kutokana na au dhidi ya dhima zote ,hasara nyingine yoyote ambayo inaweza kutokea kutokana au inayohusiana na uendeshaji au utumiaji wa akaunti hii au huduma hizi au kuvunja,kutotenda au utendaji usiotosheleza wa mteja kwa mojawapo ya kanuni na sheria hizi au vitendo hivi,makosa mawasiliano ,kutoelewana vyema ,mwenendo ,mbaya au uzembe wa mteja katika utekelezaji wa majukumu yake.
b) TANESCO SACCOS kwa ajili yoyote ile,haitawajibika kwa mteja kwa hasara yoyote isiyo ya moja kwa moja ,ya dharura ,itakayosababishwa na madhara maalumu yanayohusiana na akaunti hii au huduma hizi.
c) TANESCO SACCOS haitawajibika kwa kushindwa kokote kutekeleza jukumu lolote lililomo katika masharti haya au kwa hasara yoyote au madhara yoyote yawayo yaliyosababishwa na mteja kwa hali yoyote ile na iwe hasara hii au madhara haya yawe yanayodhaniwa kuwa ndio sababu (ya moja kwa moja au isiyo ya moja kwa moja)kwa mgogoro wowote au suala lingine lolote au hali yoyote.
d) Mteja atalipa fidia TANESCO SACCOS kama mlipaji wa hundi au hati za fedha kwa hasara yoyote au madhara ambayo TANESCO SACCOS inaweza kuingia kwa kudhamini uidhinishwaji wowote au ulipaji wa hundi ,bili au hati nyingine zilizowasilishwa kwa ajili ni malipo na udhamini huu kama unavyotolewa na TANESCO SACCOS Utachukuliwa kuwa umetolewa katika kila tukio kwa maombi ya haraka ya gharama za mteja .
e) Mteja ataifanya TANESCO SACCOS ifidiwe kwa wakati wowote dhidi ya ,na kuiepusha TANESCO SACCOS kutokana na vitendo vyote, mashauri, malalamiko, hasara, madhara gharama, faida (kabla na baada ya hukumu kwa pamoja) na gharama zikijumuisha gharama za kisheria kwa vigezo vya gharama za mwanasheria na mteja) ambazo zinaweza kuletwa dhidi ya au kuingiwa na TANESCO SACCOS katika utekelezaji wa haki za TANESCO SACCOS au kuhusiana na kanuni na sheria hizi zilizopo katika jambo hili, au ambazo zinaweza kutokea moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja nje ya au kuhusiana na TANESCO SACCOS katika utekezaji wa majukumu yake haya au kupokea maelekezo. Ikiwa ni pamoja na, lakini yasiyokomea kwenye fakisi na mawasiliano mengine ya simu au maelekezo ya kielectroniki na kuyafanyia kazi au kushindwa kutekeleza
f) Iwapo mteja anadaiwa kiasi chochote cha fedha na hajalipa kwa tarehe ipasayo ikijumuisha bila ukomo fedha zozote zinazodaiwa chini ya aya hii, mteja huyu atawajibika kulipa riba ya kiasi hicho cha pesa ambacho hakikulipwa kwa kiwango au viwango vitavyotolewa na TANESCO SACCOS mara kwa mara kutoka tarehe ambayo malipo hayo yalikuwa yanatakiwa kufanywa hadi tarehe ya malipo.
g) Mteja peke yake atawajibika katika kuhakikisha kwamba anafuata kikamilifu sheria na kanuni zozote zinazotumika katika utekelezaji wa sheria yoyote inayohusika na ufungwaji wa Akaunti yake katika TANESCO SACCOS na atasaidiana kuhakikisha ufidiwaji wa TANESCO SACCOS kutokana na vitendo vyote, mashauri, malalamiko, hasara, uharibifu, gharama (Ikiwa ni pamoja na gharama za kisheria) ambazo zinaweza kuingiwa dhidi ya au kugharamiwa na TANESCO SACCOS kutokana na kushindwa kokote kufuata sheria au kanuni yoyote ile.
h) Fidia kama ilivyotajwa itaendelea bila kujali ufungaji wa akaunti hii.

26.UDHIBITI WA DATA.
TANESCO SACCOS itapewa haki ya kutunza taarifa binafsi zilizotolewa na mteja na taarifa nyingine kuhusiana na au zinazohusu uhusiano kati ya TANESCO SACCOS na mteja kwenye kanzi data za kielectroniki, mfumo wa kawaida wa kuingiza kwenye faili au kwa njia nyingine yoyote .Tawi lolote au wakala wa TANESCO SACCOS ambalo mmiliki wa akaunti ana uhusiano inaweza kutumiwa na kusahihisha taarifa zozote muhimu zilizohifadhiwa ili kutoa huduma kwa mteja,kuepusha udanganyifu na kutengeneza upya rekodi za binafsi kuhusu mteja.

27.SIRI
TANESCO SACCOS itaendeleza na kulinda jukumu lake la usiri kuhusiana na masuala ya fedha ya mteja kwa mujibu wa Sheria ya Tanzania na Sheria za huduma ya TANESCO SACCOS zinazokubalika kimataifa
TANESCO SACCOS itatoa tu taarifa zinazohusiana na akaunti ya mteja kama ina jukumu (au inatakiwa kisheria) kufanya hivyo, au kama mteja ataomba au atatoa idhini ya utoaji wa taarifa hiyo,ama kulingana na ibara ya 5.5 au vinginevyo.

28.MAWASILIANO
28.1 Mpaka TANESCO SACCOS iwe imetoa taarifa ya anuani maalum kwa mteja ,barua yoyote notisi au hati nyingine inayohusiana na akaunti itaweza tu kuhifadhiwa kwenye TANESCO SACCOS na mteja kwenye tawi la TANESCO SACCOS ambako kimsingi mteja hufanyia biashara.
28.2 TANESCO SACCOS inaweza kumpa mteja taarifa ya aina yoyote kwa namna ambayo TANESCO SACCOS itaiona mahsusi barua yoyote, notisi au hati nyingine zilizohifadhiwa na TANESCO SACCOS kwa mteja zitachukuliwa kuwa zimehifadhiwa, kama zitapelekwa na njia ya Posta na kutumwa kwa mteja kwa anuani waliyojulishwa kwa mara ya mwisho, saa 72 baada ya kutuma nchini Tanzania, na saa 144 kwa nchi nyingine yoyote.
28.3 TANESCO SACCOS inaweza kufuatilia na kurekodi simu zilizopigwa kuhakikisha kwamba maelekezo ya mteja yamefanyika kwa usahihi na kuboresha ubora wa huduma za TANESCO SACCOS .
28.4 TANESCO SACCOS inaweza kuwasiliana na mteja kuhusu huduma nyingine za TANESCO SACCOS ambazo TANESCO SACCOS inaamini kwamba zinaweza kuwa za manufaa kwa mteja labda ikiwa mteja ataitaarifu TANESCO SACCOS kwa maandishi kwamba hapendi kupokea taarifa hizo.
28.5 Mteja bila kukawia ataijulisha TANESCO SACCOS kuhusu utokeaji wa tukio lolote ambalo litafanya TANESCO SACCOS kuvunja uhusiano wake au uhusiano wote na mteja kulingana na ibara ya 23.2.

29.HAKUNA KIZUIZI
Mteja hataanzisha au kuruhusu kujikimu , fidia yoyote ya mali au maslahi ya mtu wa tatu kuhusu au dhidi ya akaunti yoyote ya TANESCO SACCOS au fedha zozote katika jambo hili bila TANESCO SACCOS kutoa idhini kabla ,kwa njia ya maandishi

30.UHALALI WA KANUNI NA MASHARTI
Ikiwa sharti lolote katika kanuni na masharti haya au kanuni na masharti

yoyote muhimu yanayohusika yameonekana kutokuwa thabiti , sharti hilo au sehemu ya sharti hilo itachukuliwa kuwa si sehemu ya kanuni na masharti haya au kanuni ya masharti mahususi kama itakavyoonekana inafaa.Utekelezaji wa masharti yaliyobakia hautaathiriwa.

31.MATUMIZI YA KADI

31.1 TANESCO SACCOS itatoa kadi ya wateja ambao maombi yao yamekubaliwa.
31.2 Kadi itabakia kuwa mali ya TANESCO SACCOS na kuhusiana na ubatilisho ni lazima irejeshwe idaiwapo na TANESCO SACCOS .
31.3 Kadi itamwezesha mmiliki wa kadi:
a) Kutoa fedha taslim kutoka ATM yoyote ya TANESCO SACCOS, Benki ya Posta au benki yoyote iliyopo kwenye swichi ya Umoja kwa shilingi za kitanzania
b) Kubadilisha namba ya siri kwenye ATM zozote za TANESCO SACCOS au Benki ya Posta au benki yoyote iliyopo kwenye swichi ya Umoja kwa shilingi za kitanzania
c) Kupata salio la akaunti na taarifa fupiza
d) Kuendesha huduma nyingine zozote za kadi ambazo zinaweza kutolewa na TANESCO SACCOS siku hadi siku.
31.4 Utoaji wowote wa fedha kwenye ATM za TANESCO SACCOS utategemea ukomo wa kutoa kila siku.
31.5 Kadi Haitampa wala Haitamwezesha mmiliki wa kadi kuzidi ukomo wa akaunti au kutoa zaidi ya akaunti.
31.6 Rekodi za TANESCO SACCOS kwa muamala wowote au matokeo yake katika hilo utakuwa wa kuthibitisha
31.7 Matumizi yasiyo sahihi ya ATM au ya kuingiza au ya kuingiza kwa makosa namba ya siri yatasababisha uzuiaji kiautomatiki wa kadi hii,ambayo inaweza kurejeshwa kwa kwenda kwenye tawi la mteja pamoja na utambulisho sahihi.
31.8 TANESCO SACCOS Imeidhinishwa kutoa fedha kwenye akaunti ya mmiliki wa kadi kwa kiasi chote kitakachotolewa kwa njia ya kadi na namba ya siri.
31.9 Mmiliki wa kadi atalazimika kuchukua tahadhari zote kuhakikisha usalama wa kadi hii na usiri na namba ya siri wakati wote na kuepusha hasara ya au matumizi ya namba ya siri na mtu wa tatu.Wamiliki wa akaunti ya pamoja watawajibika kikamilifu katika kuhakikisha kwamba namba ya siri inajulikana tu wakati wote kwa watu walioidhinishwa ambao wanamiliki akaunti ya pamoja. Mmiliki wa kadi atawajibika kulingana na muamala wowote utakaofanywa kabla ya TANESCO SACCOS kupokea taarifa ya hasara au wizi huo.
31.10 Kama kadi itapotea au kuibiwa,mmiliki atalazimika kuijulisha TANESCO SACCOS mara moja juu ya hasara hiyo au wizi kwa maandishi au kwa njia ya simu.
31.11 Wamiliki wa akaunti na wamiliki wa kadi watabakia pamoja na mbalimbali watawajibika kwa TANESCO SACCOS kwa muamala wowote uliofanywa kwa kutumia kadi hii kabla kwa kupokewa kwa notisi ya maandishi.
31.12 Muda na tarehe ya upokeaji wa notisi ya maandishi utachukuliwa kuwa tarehe ya taarifa kwa TANESCO SACCOS
32.13 Kama ripoti ya hasara au wizi wa kadi hii utatolewa na watu wengine nje ya mmiliki ,TANESCO SACCOS haitawajibika kwa hasara yoyote itakayoingiwa na mmiliki wa kadi
31.14 Wamiliki wa kadi watalazimika kuwa na uangalizi wa kutosha kuhakikisha usalama wa kadi na usiri wa namba zao za siri wakati wote ili kuepusha hasara.
31.15 Wamiliki wa kadi watawajibika kwa madhara yatokanayo na jukumu lao linalohusu matumizi na utunzaji wa kadi hii.
31.16 TANESCO SACCOS haitawajibika na kufichuka siri kwa mtu wa tatu utokanao na matumizi ya ATM au kwa hasara yoyote,uharibifu au madhara yatayotokana na matumizi ya kadi
31.17 Wamiliki wa kadi ya pamoja ni lazima wasaini kuonyesha ridhaa yao kwa matumizi ya kadi hii na mmiliki wa kadi aliyeteuliwa na TANESCO SACCOS ya hesabu kama ilivyotokea kwenye akaunti inayotokana na matumizi hayo
31.18 Wamiliki wa Akaunti ya pamoja ambayo miamala ya kadi imetumwa watawajibika kwa pamoja na mara kwa mara kwa madhara yatakayotokana na jukumu la mmiliki wa kadi kuhusiana na matumizi na utunzaji wa kadi hii
31.19 Kadi itakuwa ya halali kisheria mpaka pale itakapoamuliwa vinginevyo kwa uamuzi wa TANESCO SACCOS
31.20 Kadi itabadilishwa kwa uamuzi wa TANESCO SACCOS katika tarehe ya kwisha kwa matumizi yake mpaka mmiliki wa kadi atoe maelekezo tofauti
31.21 Kadi itaendelea kubakia kuwa mali ya TANESCO SACCOS. TANESCO SACCOS inaweza kusimamisha au kukataa kuhuisha kadi ya tarehe yake ya kwisha kwa matumizi yake pasipo kutoa sababu yoyote
31.22 Ikiwa mmiliki wa kadi amefariki au amevunja mojawapo ya masharti yaliyo katika mkataba TANESCO SACCOS inaweza kuchukua hatua zilizo muhimu kusimamisha utumiaji wowote wa kadi hii na kufuta matumizi yake.

32.MKATABA KAMILI

Kanuni na masharti haya pamoja na kanuni na masharti maalum yanayohusika, mwongozo wa ushuru wa forodha na mkataba wowote mahsusi wa maandishi kati ya TANESCO SACCOS na mteja vinafanya mkataba kamili kati ya TANESCO SACCOS na mteja.

33. Sheria inayohusika na mamlaka ya Kisheria.

33.1 Kanuni na masharti haya, kanuni na masharti yoyote mahsusi na mkataba mahsusi wa maandishi kati ya TANESCO SACCOS na mteja itaongozwa na kutafsiriwa kwa mujibu wa sheria za Tanzania.
33.2 Mteja bila kupinga anakubali kwamba Mahakama za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zitakuwa na mamlaka ya kisheria katika kuamua kuhusu malalamiko yoyote, tofauti au mgogoro unaoweza kutokea au utakaohusu uhusiano wa TANESCO SACCOS na mteja, ikiwa ni pamoja na kanuni na masharti haya, Kanuni Masharti yoyote mahsusi na mikataba mahsusi katika masharti kati ya TANESCO SACCOS na mteja
33.3 Bila kuathiri masharti ya ibara ya 33.2 TANESCO SACCOS itakuwa na haki ya kufungua masharti dhidi ya mteja katika mahakama yoyote nyingine yenye mamlaka halali ya kisheria.

34. MALALAMIKO.

Katika tukio la kusababisha malalamiko, mteja katika tukio la kwanza atapaswa kumwandikia Meneja wa TANESCO SACCOS, iwapo mteja atakuwa hakuridhika mwenyekiti wa TANESCO SACCOS .

Nimesoma,Nimeelewa vizuri na nakubali kufuata kanuni na masharti ya hati hii.

Mahali.....Tarehe.....

Jina..... Saini.....

Kwa Matumizi ya ndani tu:
Imesainiwa mbele ya:

Jina la Ofisa _____ **Saini** _____